Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-27-970-430

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**HOJA MWENDESHA DHIDI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI NA. 032/2016**

**HUKUMU KUHUSU HOJA ZA MSINGI NA FIDIA**

**13 Juni 2023**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU**

**Arusha, tarehe 13 Juni 2023**, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (Mahakama) ilitoa hukumu katika kesi ya *Hoja Mwendesha dhidi ya Jamhuri ya Tanzania.*

Bwana Hoja Mwendesha (Mwombaji) ni mkulima na raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Nchi Inayolalamikiwa). Wakati akiwasilisha Maombi hayo, alikuwa akitumikia kifungo cha miaka thelathini (30) katika Gereza la Msalato mjini Dodoma, akiwa ametiwa hatiani kwa kosa la kumbaka mtoto wa miaka kumi na mitatu (13). Katika Maombi yaliyo mbele ya Mahakama, anapinga ukiukwaji wa haki zake kuhusiana na mwenendo wa mashauri katika mahakama za ndani.

3. Kwa mujibu wa kumbukumbu Mwombaji alitiwa hatiani kwa kosa la kumbaka na kumpa mimba msichana ambaye ni mwanafunzi mwenye umri wa miaka kumi na mitatu na baadaye kuhukumiwa kifungo cha miaka thelathini (30) na Mahakama ya Wilaya ya Misungwi.

Katika Maombi yake, Mwombaji anadai kuwa Nchi Inayolalamikiwa ilikiuka haki zake chini ya Ibara ya 3(1), na (2), 5, 7(1)(c) ya Mkataba kutokana na mwenendo wa kesi kwenye mahakama za ndani.

Nchi Inayolalamikiwa ilipinga mamlaka ya Mahakama kwa madai kuwa kinyume na Ibara ya 3(1) ya Protokali ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu kuhusu Uanzishwaji wa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu (Protokali) na Kanuni ya 26(1)(a) ya Kanuni za Mwenendo wa Mahakama (Kanuni), Maombi haya yanaitaka Mahakama kukaa kama mahakama ya rufaa ili kushughulikia masuala ya msingi kwenye kesi na sheria yaliyoamuliwa hapo awali na Mahakama ya Rufani ya Tanzania. Kwa mujibu wa Nchi Inayolalamikiwa, mapitio hayo hayako ndani ya mamlaka ya Mahakama hii.

Mahakama ilibainisha kuwa tayari imethibitisha kwamba pale ambapo madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu yanahusiana na namna mahakama za ndani zilivyotathmini ushahidi, ina mamlaka ya kuamua kama tathmini hiyo inaendana na hati za kimataifa za haki za binadamu ambazo Nchi Inayolalamikiwa ni mwanachama, ikiwa ni pamoja masharti husika ya Mkataba. Baada ya kubaini kuwa madai ya Mwombaji yanahusiana na ukiukwaji wa haki zake chini ya Ibara ya 3, 5 na 7 ya Mkataba. Mahakama iliona kuwa ilikuwa na mamlaka ya kuchunguza Maombi hayo na hivyo basi kutupilia mbali pingamizi la Nchi Inayolalamikiwa dhidi ya mamlaka ya mahakama hii.

Kuhusu mamlaka binafsi, Mahakama ilibaini kuwa Nchi Inayolalamikiwa ni sehemu ya Protokali hiyo na kwamba pia iliwasilisha, tarehe 29 Machi 2010, Tamko kwa mujibu wa Ibara ya 34(6) ya Protokali hiyo, ambapo ilikubali mamlaka ya Mahakama ya kupokea maombi kutoka kwa watu binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali yenye hadhi ya mwangalizi kwenye Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu. Mahakama pia ilibainisha kuwa tarehe 21 Novemba 2019, Nchi Inayolalamikiwa iliwasilisha kwa Mwenyekiti wa Kamisheni ya Umoja wa Afrika, hati ya kuondoa Tamko lake.

Mahakama ilisisitiza kuwa, kama ilivyokuwa katika kesi ya Andrew Ambrose Cheusi dhidi ya Tanzania, uondoaji wa Tamko lililowasilishwa kwa mujibu wa Ibara ya 34(6) ya Protokali hauna athari ya kurudi nyuma na hauathiri kesi zinazoendelea wakati wa kuwasilisha hati ya kujiondoa, kama ilivyo katika shauri hili. Mahakama pia ilibainisha kuwa uondoaji wa Tamko hilo unaanza kutumika miezi kumi na miwili (12) baada ya kuwasilisha hati ya uondoaji. Kuhusiana na Nchi Inayolalamikiwa, uondoaji huo utaanza tarehe 21 Novemba 2020. Hivyo, Mahakama iliona kuwa ina mamlaka ya binafsi ya kusikiliza kesi hiyo.

Mahakama pia iliona kuwa ina mamlaka ya muda na eneo kwani ukiukwaji ulifanyika baada ya Protokali kuanza kutumika kwenye Nchi Inayolalamikiwa na ulifanyika katika eneo lake.

Kuhusiana na kupokelewa kwa Maombi, Nchi Inayolalamikiwa iliweka mapingamizi mawili ya awali ya kupokelewa kwa Maombi. La kwanza linahusiana na kutumia kikamilfu usuluhishi wa ndani wakati la pili linahusiana na kushindwa kuwasilisha Maombi ndani ya muda stahiki baada ya kumalizika kwa usuluhishi wa ndani.
Katika pingamizi la kwanza, Nchi Inayolalamikiwa ilidai kuwa zipo taratibu za ndani za usuluhishi ambazo Mwombaji angeweza kuzifuata kabla ya kuifikia Mahakama hii. Kwa mujibu wa Nchi Inayolalamikiwa, Mwombaji alikuwa na fursa ya kuwasilisha maombi ya kutaka mapitio ya hukumu kwenye Mahakama ya Rufani. Nchi Inayolalamikiwa inadai kuwa Mwombaji pia alikuwa na fursa ya

kuwasilisha maombi ya kikatiba ya kupinga uhalali wa hukumu chini ya Sheria ya Haki za Msingi na Utekelezaji wa Wajibu.

Mahakama ilitupilia mbali hoja ya Nchi Inayolalamikiwa, ikibainisha kuwa baada ya hukumu ya Mahakama Kuu, Mwombaji alikata rufaa katika Mahakama ya Rufani, mahakama ya juu zaidi katika mfumo wa mahakama wa Nchi Inayolalamikiwa. Mahakama ilibaini kuwa Mwombaji alitumia kikamilifu usuluhishi wa ndani kwani rufaa hiyo iliipa mahakama ya ndani fursa ya kutosha kushughulikia madai yaliyotolewa na Mwombaji mbele ya Mahakama Kuu. Pia, kuhusu suala la mapitio na changamoto ya kikatiba, Mahakama ilibaini kuwa hapo awali ilitoa uamuzi kwamba hizo ni suluhu zisizo za kawaida ambazo Mwombaji halazimiki kuzitumia. Mahakama iliona kuwa Mwombaji alitumia kikamilifu usuluhishi wa ndani kwa mujibu wa Ibara ya 56(5) ya Mkataba na Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni hizi.

Nchi Inayolalamikiwa ilidai pia kuwa Maombi hayo hayastahili kupokelewa kwa sababu yaliwasilishwa kwa nje ya muda.
Katika shauri hili, Mahakama ilibainisha kuwa chini ya Ibara ya 56(6) ya Mkataba, iliyorejelewa katika Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni za Mahakama, hakuna muda maalumu ambapo kesi lazima ifunguliwe kwenye Mahakama hii. Mahakama, ilimradi muda uliowekwa ni wa kuridhisha kwa kuzingatia vigezo ambavyo vinachunguzwa kwa msingi wa kesi baada ya kesi kulingana na mamlaka ya Mahakama hii.

Katika muktadha huo, Mahakama iliona kuwa muda wa miezi sita (6) na siku nane (8) ni muda mwafaka wa kufungua shauri hilo kwa mujibu wa Ibara ya 56(6) ya Mkataba na Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni hizi. Hivyo, Mahakama inatupilia mbali pingamizi la Nchi Inayolalamikiwa kuhusu kupokelewa kwa Maombi hayo. Kwa kuzingatia masharti mengine ya kukubaliwa ambayo hayakupingwa na Pande hizo mbili, Mahakama iliona kuwa Maombi hayo ni halali na hivyo kutamka kuwa yanapokelewa.

Mwombaji anadai kuwa Nchi Inayolalamikiwa ilikiuka i) haki yake ya usawa mbele ya sheria na haki yake ya ulinzi sawa wa kisheria; iii) haki yake ya kuheshimu utu wake, na iii) haki yake ya kupata msaada wa kisheria bila malipo. Kuhusiana na madai ya kwanza ya ukiukwaji wa haki ya usawa mbele ya sheria na ulinzi sawa wa kisheria, Mahakama iliona kuwa Mwombaji hakuthibitisha madai yake. Hivyo Mahakama iliyatupilia mbali.

Kuhusiana na madai ya pili ya ukiukwaji wa haki ya utu, Mahakama pia ilibainisha kuwa Mwombaji hakutoa ushahidi wowote wa ukiukwaji huo na kwamba hakukuwa na ushahidi wowote kwenye kumbukumbu kuashiria ukiukwaji huo. Hivyo madai hayo yalitupiliwa mbali.

Baada ya kuchunguza madai ya ukiukwaji wa haki ya kupata msaada wa kisheria bila malipo, Mahakama iliona kwamba ingawa Mwombaji alishtakiwa kwa ubakaji, kosa kubwa linalostahili adhabu ya kifungo kisichopungua miaka thelathini (30), hakuna ushahidi wowote kwenye kumbukumbu kwamba alijulishwa kuhusu haki yake ya kupata msaada wa kisheria. Zaidi ya hayo, Mwombaji hakujulishwa kuwa anaweza kupata msaada wa kisheria bila malipo hata kama hawezi kumudu. Mahakama pia inabainisha kuwa Nchi Inayolalamikiwa haikupinga kuwa Mwombaji ni maskini. Kwa kuzingatia hayo, Mahakama ilibaini kuwa Nchi Inayolalamikiwa haikutimiza wajibu wake chini ya Ibara ya 7(1)(c) ya Mkataba, iliyosomwa pamoja na Ibara ya 14(3)(d) cha ICCPR, kwa kadiri ilivyokuwa, ilishindwa kumpatia Mwombaji msaada wa kisheria bila malipo katika shauri mbele ya mahakama za ndani.

Kuhusu fidia, Mwombaji aliiomba Mahakama impatie fidia kwa ukiukwaji aliofanyiwa, ifute hukumu yake, na iamuru aachiwe huru. Kuhusu fidia ya kifedha, Mahakama ilibaini kuwa ukiukwaji huo ulisababisha Mwombaji kuathirika kimaadili / kihisia na hivyo, kwa kutumia mamlaka yake ya kimahakama, inampatia tuzo Mwombaji kiasi cha Shilingi Laki Tatu (300,000) za Kitanzania kama fidia ya haki.

Kuhusiana na fidia isiyo ya kifedha, Mahakama iliona kwamba katika kesi hii, hakuna chochote kuhusiana na ukiukwaji huo kinachoonyesha kuwa kumweka Mwombaji gerezani ni uvunjifu wa haki au uamuzi wa kiholela. Mwombaji pia alishindwa kuonyesha hali ya kipekee zaidi na ya kulazimisha ili kuhalalisha kuachiliwa kwake. Kwa mantiki hiyo, Mahakama ilitupilia mbali maombi ya Mwombaji ya kutaka amri ya kutenguliwa hukumu yake na kumwachia huru.

Mahakama iliamuru kila upande ubebe gharama zake.

**Taarifa za ziada**

Taarifa zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na nakala kamili ya hukumu ya Mahakama ya Afrika, inapatikana kwenye: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0322016

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe: registrar@african-court.org

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu ni mahakama ya bara iliyoanzishwa na nchi za Afrika ili kuhakikisha ulinzi wa haki za binadamu barani Afrika. Mahakama ina mamlaka kuhusu kesi na migogoro yote iliyowasilishwa kwake kuhusiana na tafsiri na matumizi ya Mkataba, Protokali hii na hati nyingine zozote za Haki za Binadamu zilizoridhiwa na Nchi husika. Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.*